

KIAMBATISHO A



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MUHTASARI WA MATOKEO YA ROBO YA TATU (JULAI - SEPTEMBA) YA PATO LA TAIFA, 2016

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
Januari, 2017**

1. Utangulizi


Pato la Taifa ni thamani ya bidhaa na huduma zinzazozalishwa na wananchi katika kipindi husika. Pato la Taifa kwa robo mwaka hutayarishwa katika kipindi cha miezi mitatu mitatu ambavyo ni Robo ya Kwanza (Januari – Machi), Robo ya Pili (Aprili – Juni), Robo ya tatu (Julai – Septemba) na Robo ya Nne (Oktoba – Desemba).

2. Matokeo Muhimu

Mwaka 2016, Robo ya Tatu ya Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa na thamani ya Shilingi Trilioni 25.5 ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 22.7 zilizopatikana katika robo ya tatu ya mwaka 2015.

Robo ya Tatu ya Pato la Taifa mwaka 2016 kwa bei za mwaka 2007 lilikuwa Shilingi Trilioni 11.6 ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 10.8 zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Pato la Taifa katika Robo ya Tatu ya mwaka 2015 liliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 6.2 ikilinganishwa na asilimia 7.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2015.

Mchoro Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa Robo ya Tatu ya Mwaka 2015 na 2016



Ukuaji wa Robo ya Tatu ya mwaka 2016 kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi unaonesha kwamba Shughuli ya Uchimbaji Madini na Mawe iliongezeka kwa kasi kubwa zaidi ya asilimia 19.9 ikifuatiwa na Usambazaji Maji iliyoongezeka kwa kasi ya asilimia 14.5 na shughuli ya Habari na Mawasiliano iliongezeka kwa asilimia 14.3. Aidha, shughuli za kiuchumi za Kilimo na Upangishaji Nyumba ziliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 0.3 na asilimia 2.3 mtawalia. Ukuaji wa jumla wa shughuli za kiuchumi ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo, (asilimia 12.2), Uzalishaji Umeme (asilimia 11.8); na Huduma za Fedha na Bima (asilimia 8.8).

3. Ukuaji wa Uchumi katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

Miongoni mwa Nchi za Afrika Mashariki, ukuaji wa uchumi katika Robo ya Tatu ya Mwaka 2016 unaonesha kuwa, Pato la Taifa la Nchi ya Kenya liliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 6.0 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji wa Rwanda uliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 5.2 robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.9 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Uchumi wa Uganda uliongezeka kwa kasi ya asilimia hasi 0.2 robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.0 ya robo ya tatu mwaka 2015. Ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa kwa Nchi ya Burundi haujakamilika.

4. Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi

4.1 Kilimo

Shughuli za Kilimo zinajumuisha uvunaji wa mazao ya mimea na wanyama, yanayotokana na uzalishaji wa mazao ya mimea, uzalishaji na ufugaji wa wanyama, uvunaji wa mazao ya miti kutoka katika mashamba ya miti pamoja na uvunaji wa wanyama pori na mazao ya miti ya porini.


Katika kipindi husika, Shughuli za Kilimo ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 0.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Kasi ndogo ya ukuaji ilisababishwa na kuchelewa kwa mvua za vuli katika maeneo ya uzalishaji yanayopata mvua za vuli.

4.1.1 Kilimo cha Mazao

Mazao makuu ni pamoja na mahindi, mpunga, mtama/uwele, mazao mengine ya nafaka, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, mazao mengine ya mizizi, maharage, mazao ya mafuta, mboga za majani, ndizi, mazao ya matunda, korosho, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na bishara.

Ukuaji katika shughuli ya uzalishaji mazao uliongezeka kwa kasi ya asilimia hasi 2.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 8.1 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na upungufu mkubwa wa mvua za vuli kwenye maeneo ya uzalishaji yanayotegemea mvua hizi.

Mchoro Na. 2: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao katika Robo ya Tatu ya Mwaka 2015 na 2016



Baadhi ya mazo makuu yaliyochangia katika ukuaji ni Mahindi asilimia 35.3 kutoka tani elfu 1,456 katika robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi tani elfu 1,970 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Mpunga uliovunwa uliongezeka kwa asilimia 34.5 kutoka tani elfu 537 katika robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi tani elfu 722 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Maharage yaliyovunwa yaliongezeka kwa asilimia 64.2 kutoka tani elfu 106 robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi tani elfu 174 kipindi kama hicho mwaka 2016. Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 37.5 kutoka tani elfu 72 katika robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi tani elfu 99 kipindi kama hicho mwaka 2016. Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 17.9 kutoka tani elfu 39 robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi tani elfu 46 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

4.1.2 Mifugo

Uzalishaji wa mifugo na mazao yake unatokana na ufugaji wa mifugo ya kiasili na iliyoboreshwa. Mifugo hiyo ni pamoja na ng'ombe; mbuzi; kondoo; nguruwe; punda na farasi; sungura na kuku.

Ukuaji wa shughuli za mifugo ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 2.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 2.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wanyama waliovunwa pamoja na mazao yake ikiwa ni pamoja na maziwa na ngozi katika kipindi husika.

4.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusika na uzalishaji wa mazo ya misitu, ikiwa ni pamoja na magogo, mkaa, kuni, na mazao mengine ya misitu yasiyotokana na miti kama asali na nta.

Ukuaji wa shughuli za misitu uliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.5 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ilitokana na uvunaji endelevu wa mazao ya misitu.

4.1.4 Uvuuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za baharini na maji baridi, wenyе lengo la kuvua samaki na mazao mengine ya bahari.

Ukuaji wa shughuli za uvuvi ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.5 kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa mazao ya baharini na maji baridi.

5.1 Uchimbaji Madini na Mawe

Uchimbaji madini na mawe unahusisha ukusanyaji wa madini yabisi yanayopatikana kwenye uso wa dunia (kama vile makaa ya mawe na chuma), vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Ukusanyaji huu unaweza kuwa chini ya ardhi, juu ya ardhi na pia kutoka kwenye visima. Shughuli hii inajumuisha pia kazi za ziada za kuongeza thamani ya madini kama vile kusafisha, kukata na kupanga katika madaraja tayari kwa kupelekwa kwenye masoko.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka kwa kasi ya asilimia 19.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 8.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji wa shughuli hii ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya Tanzanite, chumvi, gesi asilia, dhahabu, shaba, fedha na makaa ya mawe. Uzalishaji wa gesi asilia, shaba na chumvi ulikuwa mkubwa katika kipindi hiki.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Baadhi ya Madini Kipindi cha Julai - Septemba, 2015 na 2016

Mineral	Unit	2015	2016
Tanzanite	Kg.	1,386.18	2,986.62
Chumvi	Tani	22,375.4	42,449.24
Gesi asilia	mmSFt3	8,353	11,060
Dhahabu	Kg.	10,315.26	11,592.51
Shaba	Tani	2,887,926.65	3,470,875.80
Fedha	Kg.	3,663.6	4,334.34
Makaa ya mawe	Tani	61,629.0	68,302.4

Chanzo: TPDC na Wizara ya Nishati na Madini, 2016

5.2 Uzalishaji Bidhaa Viwandani


Shughuli hizi zinajumuisha kuchakata malighafi kuwa bidhaa kwa ajili ya matumizi ya kati na ya mwisho. Bidhaa zinazotumika katika shughuli za uzalishaji viwandani ni pamoja na mazao ya kilimo, misitu, uvuvi, na bidhaa zinazotokana na uchimbaji madini na mawe.

Shughuli za Uzalishaji Bidhaa Viwandani ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.5 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 2.1 mwaka 2015. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa vinywaji, uchapaji, bidhaa za madawa na kemikali, plastiki, bidhaa za chuma, umeme, mashine na utengenezaji wa samani.

5.3 Uzalishaji Umeme

Katika kipindi cha Julai - Septemba 2016, Jumla ya umeme uliozalishwa uliongezeka kutoka Kwh milioni 1,550 mwaka 2015 hadi Kwh milioni 1,706 kipindi kama hicho mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 10.1. Wakati uzalishaji wa umeme katika mitambo ya TANESCO ukiongezeka kwa asilimia 42.3, uzalishaji wa umeme kutoka kwa wazalishaji binafsi ulipungua kwa asilimia 34.8 kama inavyooneshwa kwenye mchoro Namba 3.


Mchoro Na. 3: Uzalishaji wa Umeme (Mill. Kwh) Kipindi cha Julai - Septemba, 2012 - 2016



Shirika la Uzalishaji wa Umeme (TANESCO) lilizalisha asilimia 75.2 ya umeme wote uliozalishwa. Kiasi kilichobaki cha asilimia 24.8 kilizalishwa na wazalishaji binafsi. Umeme uliozalishwa kwa kutumia gesi asilia ulichangia zaidi ya asilimia 50 ya umeme wote uliozalishwa

katika kipindi hicho. Umeme uliozalishwa kwenye mitambo ya maji na mafuta ulikuwa asilimia 31 na asilimia 14.7 ya umeme wote mtawalia..

Mchoro Na. 4: Umeme Uliozalishwa kwa Aina ya Vyanzo Kipindi cha Julai - Septemba, 2016



Shughuli hii ya kiuchumi iliongezeka kwa asilimia 11.8 katika robo tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia hasi 1.1 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2015. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na umeme uliozalishwa hususani kutokana na chanzo cha gesi.


5.4 Usambazaji Maji

Shughuli ya kiuchumi ya usambazaji maji inahusika na kukusanya, kusafisha na kusambaza maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Shughuli hii inatekelezwa na Mamlaka za Maji Safi na Maji Taka za Miji na Manispaa hapa nchini. Maji yanayosambazwa yanatumika pia katika kazi za uzalishaji wa mazao na mifugo.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai - Septemba 2016, kiasi cha maji kilichozaishwa kiliongezeka hadi Mita za ujazo milioni 67.4 kutoka Mita za ujazo milioni 57.4 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka kwa kasi ya asilimia 14.5 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia hasi 3.9 ya ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu uliongezeka kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kuzalisha na kusambaza maji mijini.

Mchoro Na. 5: Kiasi cha Maji Kilichozaishwa Kipindi cha Julai - Septemba, 2012 - 2016



Chanzo: EWURA, 2016

5.5 Ujenzi

Shughuli ya ujenzi inajumuisha ujenzi kwa ujumla na shughuli maalumu za ujenzi wa majengo na kazi za kihandisi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 17.6 katika robo ya tatu ya mwaka 2015. Ukuaji huu ultokana na kuendelea kwa miradi ya uwekezaji katika kipindi hicho. Baadhi ya miradi iliyochangia kukua ni pamoja na mradi wa ujenzi wa daraja katika makutano ya barabara ya TAZARA, barabara ya Mafinga - Igawa, barabara ya Mwigumbi - Maswa na upanuzi wa viwanja vya Ndege vya Mwanza na Dodoma. Viashiria vya ukuaji wa shughuli za ujenzi ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji katika robo ya tatu ya mwaka 2016 uliongezeka na kufikia tani 1,052,184 kutoka tani 872,397 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2015.

5.6 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inahusisha Uuzaji wa bidhaa za jumla na rejareja kwa aina ye yeyote ya bidhaa, na utoaji wa huduma zinazohusiana na shughuli za kibiashara kwa ujumla. Pia inajumuisha matengenezo madogo madogo ya magari na matengenezo ya bidhaa za binafsi na kaya.

Shughuli ya kiuchumi ya uuza ji bidhaa za jumla na rejareja pamoja na matengenezo iliongezeka kwa asilimia 5.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.6 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ultokana na ongezeko la biashara ya uuza ji wa jumla na rejareja zilizozalishwa ndani ya Nchi.

5.7 Uchukuzi na Uhifadhi

Shughuli hii inahusika na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli, mabomba, barabara, maji na anga; pamoja na huduma za uhifadhi mizigo. Aidha, shughuli hii pia inajumuisha ukodishaji wa vifaa vya uchukuzi na madereva pamoja na usafirishaji wa barua na vifurushi.

Shughuli za uchukuzi na uhifadhi kwa robo mwaka ya tatu ya 2016 zilikua kwa kasi ya asilimia 12.2 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.7 kwa robo ya tatu ya mwaka 2015. Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilichangiwa na ongezeko la idadi ya abiria na kiasi cha mizigo iliyosafirishwa kwa barabara na reli na pia usafirishaji wa gesi asilia kupitia mabomba. Idadi ya magari ya abiria na mizigo yaliyopewa leseni iliongezeka mwaka 2015 na 2016 kutoka 11,330 mpaka 12,430 na kutoka 14,984 mpaka 22,481 mtawalia.

Jedwali Na. 2: Usafirishaji wa Gesi Asilia na Abiria Kipindi cha Julai - Septemba, 2015 - 2016

Maelezo	Kipimo	2015	2016
Mabomba	mmSFt3	8,353	11,060
Abiria - Reli	Elfu	230	1233
Mizigo - Reli	Tani Elfu	75	98

Cahnzo: TPDC na TRL

5.8 Huduma za Malazi na Chakula

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za malazi za muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma za chakula na vinywaji.

Robo mwaka ya tatu ya 2016, shughuli ya huduma ya malazi na chakula ilikua kwa kasi ya asilimia 5.5 ikilinganishwa na asilimia 6.2 robo mwaka ya tatu ya 2015. Kasi ya ukuaji wa

shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje kutoka 335,610 robo ya tatu ya mwaka 2015 hadi 369,355 robo ya tatu ya mwaka 2016.

5.9 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji vitabu na muziki, upigaji picha za video, uandaaji wa programu za video na runinga, kurekodi sauti, kuandaa na kurusha vipindi vya redio na runinga.


Shughuli za habari na mawasiliano kwa mwaka 2016 zilikua kwa kasi ya asilimia 14.3 ikilinganishwa na asilimia 13.4 mwaka 2015. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa muda wa maongezi kwa simu za mikononi na mezani na kupanuka kwa huduma za intaneti na utangazaji nchini kupitia vipindi vya redio na runinga..

5.10 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha na aina zote za bima, huduma za mifuko ya pensheni ya hiari na huduma nyingine za kifedha.

Shughuli za Fedha na Bima kwa mwaka 2016 zilikua kwa kasi ya asilimia 8.8 ikilinganishwa na asilimia 12.9 mwaka 2015. Ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana kutoka wastani wa triliioni 17.5 mwaka 2015 hadi wastani wa triliioni 17.9 mwaka 2016; kuongezeka kwa kiwango cha mikopo kutoka wastani wa triliioni 14.4 mwaka 2015 hadi wastani wa triliioni 16.1 mwaka 2016; na ongezeko la huduma zinazotolewa na makampuni ya bima.

Mchoro Na. 6: Kiwango cha Amana na Mikopo Julai – Septemba, 2015 na 2016



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

5.11 Upangishaji Nyumba

Shughuli hii inahusisha uuzaaji, ununuaji, ukodishaji na utoaji wa huduma nyingine za majengo kama vile kutathmini majengo. Shughuli hizi zinaweza kuendeshwa na mwenye jengo au kwa kukodisha na pia zinaweza kuendeshwa kwa kutoza ada au mikataba. Pia shughuli hizi zinajumuisha ujenzi wa miundo pamoja na umiliki au ukodishaji wa miundo hiyo.

Shughuli za upangishaji nyumba zilikua kwa kasi ya asilimia 2.3 robo mwaka ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 2.2 robo mwaka ya tatu ya mwaka 2015. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi hususani katika maeneo ya mijini.

5.12 Huduma za Kitaalamu; Kisayansi, Ufundu na Huduma Nyingine

Huduma hizi zinajumuisha shughuli maalumu za kitaalamu, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi ni pamoja na huduma za kisheria, kihasibu, usanifu majengo na uhandisi; uchunguzi wa kiufundi, utafiti na maendeleo; matangazo na tafiti za kibiashara; huduma nyingine za mifugo; kukodi na kukodisha mali kupitia madalali, ajira, mawakala wa usafirishaji, usafirishaji watalii na huduma za ulinzi na upelelezi; huduma za majengo na utunzaji mazingira; uendeshaji ofisi na shughuli nyingine zinazosaidia uendeshaji.

Shughuli hii ilikua kwa kasi ya asilimia 4.4 robo mwaka ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa asilimia 4.1 robo mwaka ya tatu ya mwaka 2015. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za kitaalamu; kisayansi, ufundu na huduma nyingine za kiutawala.

5.13 Utawala na Huduma Nyinginezo

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia uendeshaji wa biashara kwa ujumla. Shughuli hizi ni pamoja na kukodi na kukodisha mali kupitia madalali, ajira, mawakala wa usafirishaji, usafirishaji wa watalii na huduma za ulinzi na upelelezi; huduma za majengo na utunzaji mazingira; uendeshaji ofisi na shughuli nyingine zinazosaidia uendeshaji.

Shughuli hii ilikua kwa asilimia 8.3 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji hasi wa asilimia 4.4 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Kasi ya ukuaji unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za mawakala wa usafirishaji na wasafirishaji wa watalii Nchini kwa Kipindi husika na upangishaji majengo.

5.14 Utawala na Ulinzi


Shughuli hizi zinajumuisha kazi za kutunga na kutafsiri sheria, kazi za Bunge, ukusanyaji kodi ulinzi wa Taifa, usalama wa raia na mali zao, uhamiaji, usimamizi wa misaada kutoka nje ya Nchi na uendeshaji wa program mbalimbali za Serikali. Shughuli za mifuko ya pensheni pia sehemu ya Utawala na Ulinzi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia 3.5 katika robo ya tatu ya mwaka 2016 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.9 kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ultokana na matumizi ya Serikali katika sekta nzima ya umma.

5.15 Elimu

Shughuli hii inahusika na utoaji wa elimu katika ngazi mbalimbali katika taasisi binafsi na za umma. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2016 ukuaji uliongezeka kwa kasi ya asilimia 6.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.3 kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi na sekondari kwa mwaka 2016.

Mchoro Na. 7: Idadi ya Wanafunzi Waliodahiliwa, 2015 – 2016



5.16 Afya ya Binadamu na Ustawi wa Jamii

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya ya binadamu na ustawi wa jamii kwa watoa huduma binafsi na umma.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka kwa asilimia 5.4 katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016 kutoka asilimia 4.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa huduma bora kutoka kwa watoa huduma wa binafsi na umma katika kipindi husika.

5.17 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za vyama vya siasa, jumuiya mbalimbali za kijamii, matengenezo ya vifaa vya nyumbani ambavyo havijaainishwa katika shughuli zingine kiuchumi zilizotajwa. Pia imejumuishwa shughuli za Sanaa na Burudani na shughuli za Kaya kama Mwajiri.

Huduma nyinginezo zilikua kwa asilimia 6.9 katika kipindi cha robo mwaka ya tatu 2016 ikilinganishwa na asilimia 7.1 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi mijini na huduma za binafsi.

6. Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka 2016, kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka kwa asilimia 6.2 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2015. Shughuli za kiuchumi ambazo ziliongezeka kwa kasi kubwa ni pamoja na Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 19.9); Usambazaji Maji (asilimia 14.5); na Habari na Mawasiliano (asilimia 14.3). Aidha, shughuli za Kilimo na Upangishaji Majengo ziliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 0.3 na asilimia 2.3 mtawalia.

Katika kipindi cha kuanzia Januari – Septemba 2016, ukuaji wa Pato la Taifa uliongezeka kwa wastani wa asilimia 6.5 ikilinganishwa na asilimia 6.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2015.

**KIAMBATISHO 1: Pato la Taifa kwa Aina ya Shughuli za Kiuchumi
Kwa Bei za Mwaka 2007 – Sh. milioni**

Mwaka	Robo Mwaka	Kilimo	Uchimbaji Madini na Mawe	Viwanda	Uzalishaji Umeme	Usambaza ji Maji	Ujenzi	Biashara na Matengen ezo	Huduma za Malazi na Chakula	Usafirishaji na Uhifadhi	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2005		6,854,441	991,891	1,554,874	214,651	254,252	1,569,877	2,140,837	445,821	1,412,913	499,923	521,423
2006		7,015,537	856,307	1,686,027	195,942	259,762	1,871,175	2,343,062	461,199	1,541,551	522,575	621,071
2007		7,181,357	935,412	1,880,032	232,622	240,898	2,117,074	2,645,347	481,997	1,572,854	615,066	756,075
2008		7,720,033	843,949	2,094,035	251,361	246,507	2,323,320	2,817,146	497,897	1,601,242	688,106	898,007
2009		8,113,750	1,001,653	2,192,207	262,100	257,755	2,235,648	2,893,444	502,992	1,712,475	871,411	1,062,921
2010		8,332,436	1,074,285	2,388,391	297,238	263,336	2,466,660	3,181,783	521,540	1,896,112	1,084,423	1,197,164
2011		8,621,829	1,141,798	2,554,119	284,394	260,050	3,031,443	3,541,265	543,173	1,980,177	1,177,462	1,374,537
2012		8,901,917	1,217,823	2,659,200	293,804	267,407	3,127,824	3,675,197	579,598	2,062,518	1,439,326	1,445,140
2013		9,186,731	1,264,845	2,831,400	332,080	274,507	3,584,477	3,839,852	595,724	2,314,221	1,631,263	1,534,231
2014		9,497,468	1,383,349	3,024,323	363,110	284,755	4,088,927	4,223,837	609,111	2,603,499	1,762,116	1,699,700
2015		9,719,965	1,508,923	3,222,077	384,271	285,003	4,773,882	4,552,422	622,966	2,810,378	1,974,819	1,899,711
	1	1,949,755	242,973	373,896	52,237	63,335	378,164	545,865	110,055	323,548	111,082	109,330
2005	2	1,852,248	243,253	388,184	51,972	63,012	357,544	534,348	109,446	339,983	122,321	123,718
	3	1,496,675	249,368	395,861	52,815	64,158	407,100	531,007	113,304	372,911	131,616	140,597
	4	1,555,763	256,298	396,933	57,626	63,747	427,070	529,616	113,016	376,471	134,904	147,778
	1	1,989,464	209,432	414,884	49,080	62,785	393,304	591,810	113,123	384,390	115,366	144,177
2006	2	1,891,347	214,250	410,122	48,219	65,455	515,852	585,510	113,067	379,752	126,035	149,184
	3	1,513,095	220,418	428,435	48,860	66,227	539,251	589,218	116,972	391,945	136,158	160,123
	4	1,621,631	212,207	432,586	49,783	65,296	422,768	576,524	118,037	385,464	145,016	167,588
	1	2,016,472	224,830	452,060	55,450	59,261	524,943	676,337	116,899	367,200	134,166	176,465
2007	2	1,915,188	217,048	455,183	58,969	59,087	475,495	642,818	114,142	393,984	149,056	180,428
	3	1,570,280	248,933	479,281	57,780	61,832	513,347	656,353	127,656	407,555	160,017	192,811
	4	1,679,417	244,601	493,508	60,422	60,717	603,290	669,839	123,301	404,114	171,826	206,371
	1	2,190,770	214,072	496,685	60,854	59,816	532,435	683,395	122,902	396,807	164,738	215,189
2008	2	2,059,818	209,344	504,651	59,641	60,446	528,883	706,185	118,655	384,564	175,862	215,034
	3	1,684,388	222,701	552,022	61,836	62,784	738,155	706,022	129,063	405,912	180,744	229,781
	4	1,785,057	197,832	540,677	69,030	63,460	523,846	721,544	127,277	413,958	166,762	238,003
	1	2,318,940	237,220	526,676	62,634	64,204	525,950	725,175	122,232	416,137	210,828	258,467
2009	2	2,164,959	215,875	512,368	63,791	63,886	439,372	689,476	118,460	411,991	217,709	258,680
	3	1,776,543	271,890	580,104	66,369	65,036	597,526	731,407	132,041	420,261	224,704	267,741
	4	1,853,308	276,668	573,060	69,306	64,629	672,800	747,386	130,260	464,086	218,171	278,033
	1	2,394,044	251,980	586,720	67,201	63,671	514,291	781,389	125,901	465,146	254,624	276,086
2010	2	2,231,501	263,836	564,094	72,666	66,346	598,676	776,415	124,135	430,481	248,876	291,538
	3	1,804,662	273,380	630,599	78,863	67,123	658,987	787,794	137,349	473,099	261,958	307,175
	4	1,902,229	285,089	606,978	78,507	66,196	694,707	836,185	134,156	527,387	318,966	322,365
	1	2,467,957	278,595	622,020	70,324	62,893	686,636	857,567	130,605	513,838	252,722	331,577
2011	2	2,299,006	273,497	621,417	72,674	64,811	725,996	873,889	129,862	469,234	276,613	344,236
	3	1,883,775	299,696	659,510	67,474	65,332	805,925	887,954	142,663	535,987	306,145	349,879
	4	1,971,090	290,010	651,171	73,922	67,014	812,886	921,855	140,043	461,118	341,982	348,845
	1	2,553,682	299,575	644,172	65,897	64,538	737,795	936,096	136,256	535,745	340,049	350,415
2012	2	2,376,574	294,749	643,721	71,603	66,649	675,966	906,822	134,806	488,756	336,221	354,275
	3	1,940,198	312,618	684,004	75,929	68,985	835,376	900,338	156,463	534,530	378,168	365,472
	4	2,031,264	310,881	687,302	80,374	67,235	878,687	931,940	152,072	503,488	384,889	374,978
	1	2,651,679	280,573	673,407	76,440	65,227	795,294	954,119	145,186	602,357	348,979	371,188
2013	2	2,446,896	304,815	682,253	81,738	67,241	764,108	945,687	139,656	474,233	396,330	368,410
	3	1,975,146	323,060	754,908	83,765	64,246	971,592	960,388	155,894	637,938	409,927	390,143
	4	2,113,009	356,397	720,832	90,137	77,793	1,053,485	979,658	154,987	599,693	476,027	404,490
	1	2,741,616	335,939	728,555	89,874	65,702	965,378	1,055,335	150,154	690,955	408,493	412,743
2014	2	2,549,443	324,258	750,821	80,688	70,652	1,050,398	1,062,405	143,878	519,985	469,334	420,590
	3	2,059,715	339,767	802,505	94,791	72,397	964,937	1,081,514	156,256	722,429	462,662	429,588
	4	2,146,694	383,386	742,441	97,756	76,003	1,108,215	1,024,582	158,823	670,131	421,626	436,779
	1	2,688,508	337,813	800,465	99,024	70,695	1,189,013	1,132,737	148,718	791,045	460,591	460,092
2015	2	2,501,555	360,548	789,494	95,611	67,884	1,189,229	1,163,862	145,280	568,897	524,710	462,704
	3	2,164,080	367,051	819,495	93,730	72,450	1,134,980	1,141,609	165,963	770,922	524,697	484,974
	4	2,365,822	443,512	812,822	95,906	73,973	1,260,659	1,114,214	163,096	679,514	464,821	491,941
	1	2,759,638	359,736	859,988	104,940	68,956	1,240,132	1,197,919	146,808	853,282	522,175	522,356
2016	2	2,581,199	434,299	861,240	102,425	70,827	1,296,467	1,223,973	148,952	742,858	590,958	520,535
	3	2,170,557	440,045	856,102	104,816	82,989	1,213,131	1,208,743	175,020	865,146	599,756	527,457
	4											

**KIAMBATISHO 1: Pato la Taifa kwa Aina ya Shughuli za Kuchumi
Kwa Bei za Mwaka 2007 – Sh. milioni**

Mwaka	Robo Mwaka	Utawala na Ulinzi	Huduma za Kitalamu; Kisayansi; Ufundu na Huduma Nyingine	Huduma za Uwakala kwenye Utawala	Upangishaji Nyumba	Elimu	Afya ya Binadamu na Ustawi wa Jamii	Huduma Nyingine za Jamii	Ushuru wa Mabenki	Jumla ya Ongezeko la Thamani	Tofauti ya Kodi na Ruzuku	Pato la Taifa katika Bei ya Soko
2005		2,004,799	255,207	758,935	1,552,218	697,902	372,635	397,359	-240,213	22,259,746	1,343,348	23,582,244
2006		1,998,309	284,161	777,070	1,575,883	751,689	409,553	416,858	-296,431	23,291,301	1,390,011	24,681,311
2007		2,179,164	318,677	793,110	1,601,266	851,208	438,415	439,318	-331,002	24,948,888	1,821,544	26,770,432
2008		2,042,643	416,091	778,586	1,628,117	932,429	462,620	462,322	-353,602	26,350,803	1,909,825	28,260,633
2009		2,027,532	481,737	781,579	1,656,750	1,017,818	497,047	483,685	-424,177	27,928,327	2,153,392	29,781,719
2010		1,926,209	625,810	849,168	1,687,264	1,082,540	513,696	510,816	-457,867	29,441,005	2,234,499	31,675,504
2011		2,231,564	655,947	892,397	1,719,706	1,143,385	541,093	540,572	-561,275	31,673,636	2,505,661	34,179,297
2012		2,435,459	617,853	1,104,372	1,754,126	1,228,099	602,632	576,516	-568,183	33,420,626	2,515,833	35,936,459
2013		2,625,280	651,358	1,239,495	1,790,574	1,280,673	655,881	609,052	-568,580	35,673,045	2,873,500	38,546,546
2014		2,728,183	654,930	1,313,618	1,829,107	1,341,507	709,310	644,135	-623,558	38,137,426	3,093,939	41,231,365
2015		2,854,132	699,556	1,375,562	1,869,782	1,425,992	742,629	682,024	-696,521	40,708,373	3,391,850	44,100,223
	1	472,785	62,068	124,510	385,932	174,056	91,005	97,540	-55,406	5,612,730	338,830	5,951,560
2005	2	497,055	63,496	199,875	387,329	174,056	91,821	98,746	-55,810	5,642,598	328,022	5,970,620
	3	544,825	57,088	225,913	388,753	174,896	93,567	99,943	-62,287	5,478,108	347,985	5,826,093
	4	490,134	72,555	208,636	390,205	174,896	96,243	101,131	-66,710	5,526,310	328,511	5,854,820
	1	438,432	52,194	142,646	391,663	186,010	99,096	102,300	-69,249	5,810,928	335,863	6,146,790
2006	2	419,166	78,971	199,875	393,190	186,010	101,569	103,501	-70,885	5,909,590	339,551	6,249,141
	3	567,618	79,918	225,913	394,724	189,835	103,625	104,815	-78,046	5,799,101	361,937	6,161,039
	4	573,094	73,678	208,636	396,266	189,835	105,263	106,242	-78,250	5,771,682	352,659	6,124,342
	1	559,937	70,820	163,719	397,875	204,241	106,996	107,399	-78,888	6,336,183	482,692	6,818,875
2007	2	538,293	83,741	222,780	399,493	204,241	108,895	108,018	-79,612	6,247,249	424,734	6,671,983
	3	568,232	76,559	215,149	401,126	221,363	110,553	111,848	-84,257	6,096,417	469,618	6,566,035
	4	512,702	87,956	191,462	402,772	221,363	111,971	112,053	-88,245	6,269,039	444,500	6,713,539
	1	497,137	99,527	171,740	404,446	227,443	113,171	113,529	-88,966	6,675,689	400,282	7,075,972
2008	2	459,413	114,993	200,495	406,149	227,443	114,474	113,930	-85,049	6,574,933	428,583	7,009,516
	3	533,633	102,641	191,790	407,881	238,772	116,307	116,988	-88,873	6,592,546	611,892	7,204,438
	4	552,460	98,930	214,562	409,641	238,772	118,668	117,874	-90,714	6,507,640	469,068	6,976,708
	1	498,744	74,393	224,701	411,430	248,934	121,408	118,288	-105,192	7,061,169	493,993	7,555,162
2009	2	504,913	87,108	168,148	413,249	248,934	123,924	118,857	-103,714	8,717,984	494,266	7,212,250
	3	534,029	110,666	214,223	415,097	259,974	125,520	122,814	-107,678	6,808,265	581,218	7,389,483
	4	489,846	209,570	174,508	416,974	259,974	126,196	123,725	-107,592	7,040,909	583,915	7,624,824
	1	423,272	156,052	186,784	418,881	264,061	126,637	124,735	-104,966	7,376,508	556,893	7,933,401
2010	2	381,800	172,529	157,880	420,818	264,061	127,458	125,809	-111,253	7,207,665	536,594	7,744,258
	3	544,530	140,402	193,925	422,784	277,209	128,834	129,798	-117,291	7,201,179	561,961	7,769,140
	4	576,607	156,827	310,579	424,781	277,209	130,767	130,474	-124,357	7,655,653	579,051	8,234,704
	1	540,666	144,903	196,431	426,809	280,400	131,988	131,956	-130,978	7,996,910	565,256	8,562,166
2011	2	579,198	181,417	188,930	428,867	280,400	133,000	133,432	-139,352	7,937,127	599,401	8,536,527
	3	561,429	163,477	233,716	430,955	291,292	135,779	137,169	-146,198	7,911,962	669,463	8,481,425
	4	550,271	166,149	273,320	433,075	291,292	140,326	138,014	-144,747	7,927,637	671,541	8,599,178
	1	597,903	146,312	268,880	435,226	296,509	145,063	139,816	-138,305	8,555,824	613,686	9,169,510
2012	2	581,513	185,896	234,700	437,409	296,509	149,080	141,317	-140,351	8,236,215	598,151	8,834,365
	3	647,223	172,470	315,767	439,623	317,541	152,666	147,419	-143,954	8,300,833	650,258	8,951,091
	4	608,821	113,176	285,024	441,868	317,541	155,823	147,963	-145,573	8,327,754	653,738	8,981,492
	1	657,594	181,801	336,203	444,146	311,709	158,970	149,239	-134,175	9,069,936	676,311	9,746,247
2013	2	625,943	170,967	289,814	446,456	311,709	162,293	149,743	-137,274	8,691,017	665,303	9,356,320
	3	671,525	154,930	329,159	448,799	328,627	165,626	154,308	-146,844	8,832,538	766,340	9,598,878
	4	670,218	144,261	284,319	451,174	328,627	168,972	155,763	-150,286	9,079,555	765,547	9,845,102
	1	643,849	181,264	378,990	453,582	328,498	172,359	158,273	-146,125	9,815,435	731,260	10,546,695
2014	2	652,208	183,334	328,326	456,023	328,498	175,742	158,746	-152,603	9,572,727	726,799	10,299,526
	3	738,224	137,967	272,904	458,497	342,255	179,019	162,083	-160,029	9,317,479	833,188	10,150,667
